# LUGHA MKAKATI KATIKA MAWASILIANO YA *CHOKORAA*

**Ruth M. Binyanya, Ayub Mukhwana & Samuel M. Obuchi**

**Ikisiri**

*Makala hii inachunguza matumizi ya lugha mkakati katika mawasiliano ya chokoraa. Chokoraa huishi mitaani na hupitia changamoto mbalimbali zikiwamo unyanyapaa na ukosefu wa chakula. Kwa hali hii basi, chokoraa hufanya kazi kama vile kuwabebea wafanyabiashara wadogo bidhaa za kuuza na kuosha magari. Vile vile, chokoraa, wakati mwingine, huomba msaada kutoka kwa wanakundi-nje. Hali hizi mbalimbali ndizo huwafanya chokoraa kutumia lugha mkakati na kwa mitindo mbalimbali ili kutimiza nia zao za wakati husika. Data iliyokusanywa kuhusiana na mada hii inaonesha kuwa chokoraa hutumia lugha kutegemea muktadha wa mawasiliano. Tumebaini kuwa chokoraa hutumia lugha mkakati kwa kutumia mbinu kama vile kuchanganya ndimi, uradidi, matumizi ya majina yanayorejelea Mungu na vile vile matumizi ya lugha ya matusi kwa nia ya kupambana na unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje. Kwa kufuata mkabala wa isimujamii, makala hii inaonesha kuwa chokoraa hutumia lugha mkakati ili kukidhi mahitaji yao ya wakati husika. Makala hii ni ya uchambuzi ubora na hivyo basi yalitumia data ambayo ilituwezesha kushughulikia mada hii. Data ambayo imetumiwa katika makala hii ilikusanywa na Ruth Binyanya baina ya Januari-Agosti, 2020 mtaani Mathare, jijini Nairobi kwa ajili ya tasnifu yake ya uzamivu ambapo alishughulikia matumizi ya lugha mkakati katika kutimiza nia mbalimbali za wanafamilia wa mitaani.*

## Utangulizi

Maisha ya mitaani huhusishwa na changamoto mbalimbali zikiwamo unyanyapaa, ukosefu wa chakula na malazi. Changamoto hizi huweza kusuluhishwa kwa njia mbalimbali na hivyo basi uteuzi na matumizi ya lugha ya *chokoraa* ni msingi muhimu wa kuwawezesha kutimiza nia zao za wakati husika. *Chokoraa* hupata riziki yao kwa kufanya kazi kama vile kuosha magari na vile vile kuomba msaada kutoka kwa wanakundi-nje (Suda, 1997). Hii ina maana kuwa *chokoraa* huwategemea watu wa makundi-nje ili kupata riziki yao. Hivyo basi, *chokoraa* wanapaswa kuteua na kutumia lugha kwa namna itakayowawezesha kufanikisha nia zao za wakati husika. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa uteuzi wa lugha na matumizi ya lugha husika ni muhimu katika kufanikisha nia za wakati husika za *chokoraa*. Matumizi ya lugha fulani huchochewa na muktadha wa mazungumzo kama asemavyo Maleki (2007) kuwa watu hutumia

lugha kwa mtindo mahususi kutegemea muktadha. *Chokoraa* jijini Nairobi, kama walivyo binadamu wengine wote huwa na matakwa mbalimbali. Matakwa yao ya wakati husika huwafanya kuteua na kutumia lugha husika kwa mtindo mahususi ili kuzitimiza ipasavyo.

**Muktadha na mbinu za kimkakati katika mawasiliano**

Dhana *mkakati wa kimawasiliano* iliasisiwa na Selinker (1972). Selinker (keshatajwa) aliitumia dhana hii wakati alipokuwa akirejelea mojawapo ya michakato mitano ambayo wanaojifunza lugha ya pili hupitia. Watafiti kama Varadi (1973) na Tarone (1977) pia waliitumia dhana mkakati wa kimawasiliano walipokuwa wakishughulikia ujifunzaji wa lugha ya pili. Mkakati unaorejelewa hapa ni ule ambao huwawezesha baadhi ya watu kuwa na umilisi wa lugha mbili huku wengine wakiwa na ugumu wa kutumia lugha ya pili. Kwa upande mwingine, Yang & Gai (2010) walishughulikia mkakati wa kimawasiliano kwa kuchunguza umilisi wa lugha ya Kiingereza kwa Wachina. Watafiti hawa waliangalia mikakati iliyotumiwa na Wachina kujifunza Kiingereza na mtazamo wao kuhusu mkakati husika. Maritza (2016) anasema kuwa mikakati ya kimawasiliano katika kutumia lugha ya pili huwa kama vile: kutokamilisha usemi, kubadilisha msimbo, utohozi, kuomba msaada kutoka kwa wazawa wa lugha husika, kurudia maneno na vile vile kujirekebisha anaposema neno fulani vibaya. Watafiti hawa wameangalia mikakati ya kimawasiliano kwa watumiaji wa lugha ya pili. Watafiti hawa wameonesha kuwa wakati wa kujifunza lugha ya pili, watu hutumia mikakati mbalimbali kwa nia ya kufidia msamiati wasioujua katika lugha husika. Kwa hali hii watumiaji wa lugha ya pili huweza kubobea katika lugha husika baada ya kutumia mikakati mbalimbali.

Dhana ya *lugha mkakati* katika makala hii inatumiwa kwa maana ya namna *chokoraa* wanavyowasiliana katika miktadha anuai, kwa kutumia lugha tofauti tofauti na kwa mitindo anuai ili kutimiza nia zao za wakati husika. Lugha mkakati hutumiwa na *chokoraa* kwa namna ambayo huwatambulisha wao kama kikundi mahususi cha kijamii. *Chokoraa* huwasiliana pia na watu wa kundi-nje hasa wanapoomba kazi au msaada wa pesa. Mawasiliano ya aina hii huwafanya *chokoraa* kuteua lugha na kuitumia kwa namna itakayowawezesha kutimiza nia zao. Ni kwa misingi hii ambapo tulishughulikia matumizi mbalimbali ya lugha mkakati kama inavyotumiwa na *chokoraa* wa mtaa wa Mathare, jijini Nairobi. Mikakati ambayo

tulishughulikia katika makala hii ni kuchanganya ndimi, uradidi, matumizi ya lugha inayorejelea majina ya Mungu, na lugha ya matusi na kuwadhalilisha wanakundi-nje.

*Chokoraa* ni watu wanaoishi mitaani kwa sababu kama vile uyatima na ukosefu wa malezi mema kutoka kwa wazazi wao. Warambo (2011) na Muriira (2016) wanasema kuwa *chokoraa* hutumia Sheng' kwa nia ya kuficha siri dhidi ya wanakundi-nje. Hali hii inaashiria matumizi ya lugha mkakati kwa sababu upo wakati ambapo *chokoraa* hutumia msimbo pana hasa wanapoomba kazi au msaada wa kifedha. Hii inaonesha kuwa *chokoraa* huchagua lugha ipi itumike wapi na vipi. *Chokoraa* huteua na kutumia lugha mkakati ili waweze kutimiza matakwa yao ya wakati maalumu. *Chokoraa* huwa wa jinsia ya kike na ya kiume na wote hupitia changamoto mbalimbali mitaani. Njiru (2005) anasema kuwa *chokoraa* wa jinsia ya kike hupitia changamoto mbalimbali zikiwamo kudhulumiwa kimapenzi na kutunga mimba zisizopangwa. Changamoto hizi huwafanya kutumia lugha kwa namna mahususi kutegemea nia zao za wakati husika. Hali ya mtu ni mojawapo ya viamuzi vya matumizi ya lugha. Kwa hivyo basi, *chokoraa* hutumia lugha inayowiana na hali zao za wakati husika. Mazingira ya mitaani ambamo *chokoraa* huishi huwafanya kuwasiliana kwa namna maalumu ikilinganishwa na watu wengine ambao huishi nyumbani. Tofauti hii ya kimawasiliano hutokana na tofauti ya kimazingira na hali ambazo huwakumba watu wa makundi mbalimbali ya kijamii.

**Mbinu za utafiti**

Data ambayo imetumiwa katika makala hii ilikusanywa kwa ajili ya tasnifu ya Uzamivu, mwaka wa 2020 baina ya mwezi wa Januari na Agosti katika maeneo mbalimbali ya mtaa wa Mathare, jijini Nairobi ambapo ilishughulikia matumizi ya lugha mkakati katika kutimiza nia mbalimbali za *chokoraa*. Mtafiti alipata idhini ya kukusanya data kutoka kwa chifu wa eneo la Mathare. Data hiyo ilitumika katika makala hii ili kuonesha matumizi ya lugha mkakati katika mawasiliano ya *chokoraa* kwa nia ya kuwawezesha kutimiza nia zao. Mtafiti alitumia sampuli ya uongezeaji-kadiri kukusanya data yake. Kwa mujibu wa Christopoulos (2010), sampuli ya uongezeaji-kadiri ni mtindo wa kukusanya data kwa kuchagua mtu mmoja kutoka kwa watafitiwa ili kumuongoza mtafiti kwa wanakundi-ndani wengine. Mtindo wa kutumia sampuli

ya uongezeaji-kadiri ulikuwa faafu kwa sababu *chokoraa* wa Mathare huwa wamejipanga katika familia za kupanga na hivyo basi, familia moja ilitutambulisha kwa familia nyingine. Hili lilituwezesha kupata data kutoka kwa watafitiwa tofauti tofauti na kwa wakati tofauti. Mtafiti alitumia pia mbinu ya kurikodi mawasiliano ya moja kwa moja na *chokoraa*. Mawasiliano yalirikodiwa kwa kutumia kinasa sauti cha kidijitali. Wakati wa kuwasilisha data, tuliisikiliza, tukaiandika na hatimaye kuichanganua kwa njia ya kinathari. Tuliwarejelea watafitiwa wa utafiti huu kwa kutumi nambari kama vile Mtu 1 katika kila mawasiliano huku tukiwarejelea wanakundi-nje kwa kazi wanazozifanya kama vile mtafiti.

## Matumizi ya lugha mkakati katika mawasiliano ya *Chokoraa*

*Chokoraa* huwasiliana na watu mbalimbali na hivyo basi, wao huteua na kutumia lugha husika kwa mtindo utakaowawezesha kutimiza nia zao za wakati husika. Mitindo tofauti ya mawasiliano ndiyo inarejelewa kama matumizi ya lugha mkakati katika makala hii. Mitindo hii tofauti ya matumizi ya lugha ndiyo tunaiangalia katika vijisehemu vifuatavyo:

### Kuchanganya ndimi

Mtindo wa kuchanganya ndimi ni miongoni mwa mbinu ambayo hutumiwa na *chokoraa* kwa nia ya kukabiliana na maisha ya mitaani. Dhana ya kuchanganya ndimi katika makala hii ina maana ya kutumia lugha zaidi ya moja katika mawasiliano husika. Tumebaini kuwa *chokoraa* hutumia Sheng’ na Kiswahili zaidi ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza. *Chokoraa* huchopeka maneno ya Kiingereza hapa na pale katika mawasiliano yao. *Chokoraa* huchanganya ndimi katika mawasiliano yao kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo ya eneo la Kosovo 3B:

1. Mtu 1: **Sasa msupa** (*mrembo*), **umepotea**
2. Mtafiti: **Aaah, sijapotea ni shughuli**
3. Mtu 1: **Najua, si ulisema wewe ni student** (*mwanafunzi*) **lakini nipe kambao** (*shilingi ishirini*) **nibuy** (*ninunue*) **kakitu**
4. Mtafiti: **Leo hujaangukia kakitu**?
5. Mtu 1: **Eeeh, niko maubao** (*njaa*) **hata nayasikilia hapa kwa mgongo**

Lugha katika diskosi hii imetumika kimkakati ambapo **Mtu 1** amechanganya ndimi kwa kutumia maneno ya Kiswahili, Sheng' na Kiingereza. Maneno kama vile **msupa**, **kambao** na **maubao** ni maneno ya Sheng' ambayo yametumiwa kwa nia mahususi ya kupata msaada wa kifedha kutoka kwa mtafiti. Neno **msupa** limetumika kimkakati kama njia ya kumsifu mtafiti. Matumizi ya neno la kusifu mtu ni mkakati muhimu wa kutimiza lengo la kuvuta nadhari ya mzungumziwa. *Chokoraa* anachanganya ndimi anaposema kuwa ˝**…..wewe ni student lakini nipe kambao nibuy kakitu.**‟ **Mtu 1** ametumia neno la Sheng' «**kambao»** kwa kuamini kuwa lina uzito zaidi ikilinganishwa na neno husika la Kiswahili. Neno **kambao** limetumika kimkakati kuonesha udogo na ufinyu. Matumizi ya kiambishi awali **ka**- cha Kiswahili kwa neno la Sheng' **mbao**, kwa maana ya shilingi ishirini na ambayo kulingana na wao ni pesa ndogo kwa wanakundi-nje ni mkakati tosha wa kutimiza nia ya kupata msaada wa kifedha.

Neno **mbao** pia limetumiwa kama kifupisho ikilinganishwa na kutumia maneno mawili ya Kiswahili, 'shilingi ishirini'. Mbinu ya iktisadi ya lugha inatumika hapa kimkakati kwa nia ya kurahisisha mawasiliano kwa kutumia maneno ya Sheng' ambayo yanachukua mkondo wa kuwa na neno moja kwa maneno mawili au zaidi ya Kiswahili. *Chokoraa* huwa na nia ya kuzungumza na wanakundi-nje wengi ili kupata msaada kutoka kwa watu wengi iwezekanavyo. Hii ndiyo sababu watafitiwa kutumia mbinu ya iktisadi ya lugha ili kupunguza muda wa mawasiliano na mtu mmoja. Hapa mkakati unaodhihirika ni wa iktisadi ya lugha na unajitokeza kwa kutumia Sheng' badala ya maneno mawili ya Kiswahili.

Neno **maubao** ni la Sheng' na limetumiwa na mtafitiwa kwa nia ya kuzua athari inayokusudiwa kwa mzungumziwa anaposema kuwa «**Eeeh, niko maubao hata nayasikilia hapa kwa mgongo**.» Neno **maubao** linatumiwa kimkakati kwa kuwa lina uzito zaidi ya neno 'njaa' la Kiswahili. Kiambishi awali **ma**- kimetumika kurejelea wingi ikilinganishwa na neno njaa la Kiswahili ambalo halibadiliki katika hali ya umoja wala katika wingi. Nia ya *chokoraa* huyu ni kuonesha wingi ili kuibua hisia za huruma kutokana na kina cha njaa yake kwa mtafitiwa. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa *chokoraa* huchanganya ndimi kama mkakati wa kutimiza nia zao za kupata msaada kutoka kwa wanakundi-nje.

*Chokoraa* wa Mathare hupendelea matumizi ya Sheng' kisha kuhamisha ndimi kwa Kiswahili na Kiingereza wanapozungumza wao kwa wao. Watafitiwa hawa hutumia Kiswahili zaidi ikilinganishwa na Kiingereza katika mawasiliano na hasa baina yao na wanakundi-nje kisha kuchanganya na Sheng' hapa na pale. Hata hivyo, *chokoraa* huyatumia maneno ya Sheng' zaidi katika mawasiliano baina yao huku wakitia maneno ya Kiswahili. Vile vile wao huchopeka maneno ya lugha ya Kiingereza kwa kuyachanganya na viambishi vya Kiswahili. *Chokoraa* huchanganya ndimi kama mkakati wa kutaka kujieleza ipasavyo na kisha kutimiza nia zao za wakati husika. Mawasiliano yafuatayo ni ya *chokoraa* wa Mathare katika eneo la Gitathuru na yanadhihirisha matumizi ya lugha ya wanakundi-ndani:

1. Mtu 1: **Oya, oya (***vipi***).**
2. Mtu 2: **Oya, rada bro (***Namna gani ndugu***)?**
3. Mtu 1: **Niko bie (***salama***), sasa sijakushow (***sijakuambia***)**
4. Mtu 2: **Nipeleke na rieng' (***nieleze basi nijue***)**
5. Mtu 1: **Unacheki kale kachuom ketu (***unaona ule ujia wetu***)?**
6. Mtu 2: **Nakupata bro (***ndugu***)**
7. Mtu 1: **Nilikuwa nateremka na ile mbogi (***kundi***) yangu, kufika chini, tukacheki mayeng's (***warembo***). Kama kawa sisi na ile form (***mpango***) yetu tukataka kuwapiga ngeta (***kuwaibia***), msee kumbe mangoko (***warembo***) hawakutaka ngori (***shida***).**

Diskosi hii inadhihirisha matumizi ya lugha mkakati ambapo *chokoraa* wametumia Sheng' zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Mkakati wa lugha uliotumika hapa ni matumizi ya Sheng' kwa nia ya kuficha siri dhidi ya wanakundi-nje waliokuwa karibu. *Chokoraa* hawa wanazungumzia namna wao wanavyowaibia wanakundi-nje na ndiyo maana wanatumia lugha inayoeleweka na wanakundi-ndani kwa nia ya kupunguza chukulizi hasi dhidi yao. *Chokoraa* huwa hawataki kuchukuliwa kama wakora na ndiyo maana wanatumia lugha ya kuficha siri dhidi ya wanakundi-nje hasa ikizingatiwa kuwa wao huwaomba kazi na pia huwategemea kwa msaada wa pesa. **Mtu 1** anazungumza kwa kutumia Sheng' ili wanakundi-nje wasijue maeneo ambayo wao hujificha wanapoendeleza uhalifu wao kama inavyobainika anaposema kuwa

«**Unacheki kale kachuom ketu.**» Neno **kachuom** limetumika kwa maana ya njia ili wanakundi-nje wasijue sababu ambayo huwapeleka *chokoraa* wa Mathare katika njia hiyo husika. *Chokoraa* pia wametumia maneno mawili -**mayeng's** na **mangoko** kurejelea wasichana. Maneno haya yametumika kimkakati kwa kuwa wanaficha siri kuhusu watu ambao wao huwaibia zaidi. Huu ni mkakati wa kutumia maneno mawili au zaidi kurejelea kitu kile kile kwa nia ya kuficha siri.

Neno **form** ni la Kiingereza ila hapa limetumika kwa maana tofauti na maana yake halisi. Neno hili lina maana ya 'mpango' kwa mujibu wa muktadha wa mawasiliano. Maneno haya yametumika kimkakati ili kuficha maana yake halisi kwa wanakundi-nje na hili ni jambo ambalo huwawezesha kuchukuliwa kwa njia chanya ilhali wao huendeleza wizi. *Chokoraa* hutumia lugha ya kuwatenga wanakundi-nje kwa nia ya kupunguza chukulizi hasi dhidi yao. Ingawa hivyo, upo wakati ambapo *chokoraa* hulazimika kutumia msimbo pana ili waweze kueleweka na wanakundi-nje. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa muktadha ni kichocheo cha uteuzi na matumizi ya lugha.

*Chokoraa* hutumia lugha mbalimbali kwa mitindo anuai kutegemea malengo yao ya wakati husika. Kiswahili hutumiwa zaidi katika mawasiliano baina ya *chokoraa* na wanakundi-nje kwa kuwa kinaeleweka na ni lugha sambazi jijini Nairobi. *Chokoraa* wa Mathare wana mazoea ya kutumia maneno machache ya Sheng' wanapowasiliana na wanakundi-nje. Maneno haya hutumiwa kimkakati kwa kuwa huchukuliwa kuwa na uzito na yenye athari zaidi kuliko maneno ya Kiswahili. *Chokoraa* hutumia mikakati mbalimbali na ambayo itawawezesha kutimiza nia zao za wakati husika. Kisehemu kifuatacho kinaangalia mkakati wa uradidi utumiwao na *chokoraa* pia.

**Matumizi ya uradidi**

Uradidi ni mtindo wa kimawasiliano ambao hutumiwa na *chokoraa*. Uradidi ni mbinu ambayo inatumiwa na *chokoraa* kimkakati. Uradidi katika makala hii una maana ya kutumia neno fulani zaidi ya mara moja katika mawasiliano. *Chokoraa* hutumia mkakati wa uradidi wanapotaka kutimiza nia ya kupewa msaada na wenzao kama inavyobainika katika mawasiliano yafuatayo ya eneo la Gitathuru:

1. Mtu 1: **Niaje bro (***ndugu***)?**
2. Mtu 2: **Poa brathe (***ndugu***), rada (***mpango***)?**
3. Mtu 1: **Niko wire (***sina pesa***) mbaya, niko wire brathe (***sina pesa ndugu***).**
4. Mtu 2: **Hujaacha umaungoto (***uvivu***) brathe (***ndugu***).**
5. Mtu 1: **Wacha hizo, cheza ki-wewe, cheza…….**
6. Mtu 2: **Nicheze ki-mimi aje?**
7. Mtu 1: **Nataka tu ya kindukulu (***dawa za kulevya***)**
8. Mtu 2: **Huna hata ngovo (***shilingi kumi***) ukashikishe (***ukalewe***)?**
9. Mtu 1: **Niwahi tu blue, blue (***shilingi ishirini***) tu brathe (***ndugu***)**

Matumizi ya uradidi yanayojitokeza katika mawasiliano haya yanaonesha uzito wa uhitaji wa **Mtu 1**. Mbinu ya uradidi inaonesha msisitizo na inatumiwa na **Mtu 1** ili kutimiza nia ya kupata pesa kutoka kwa mwenzake. **Mtu 1** anarudia maneno kama vile **niko wire** na **blue**. Maneno haya yamerudiwa kimkakati. *Chokoraa* anarudia maneno **niko wire** kwa nia ya kusisitiza kuwa hana pesa kabisa. Neno **blue** limerudiwa kwa nia ya kuonesha kuwa anahitaji pesa kidogo tu, yaani shilingi ishirini pekee. Matumizi ya uradidi katika mazungumzo haya yanamwezesha mtafitiwa kupewa shilingi ishirini alizotaka. Kwa hali hii, uradidi wa maneno unakuwa mkakati muhimu wa kupata pesa kutoka kwa mwanakundi-ndani mwenzake.

**Matumizi ya majina ya kurejelea Mungu kama mkakati wa kukabiliana na unyanyapaa**

Mazingira ya mitaani wanakoishi *chokoraa* huhusishwa na uchafu na hii ndiyo maana baadhi ya wanakundi-nje huwaepuka. *Chokoraa* hukabiliana na unyanyapaa kwa namna mbalimbali kama vile kurejelea Mungu na vile vile matumizi ya lugha ya kuwadhalilisha wanakundi-nje. Katika kisehemu hiki tunaangalia matumizi ya maneno yanayorejelea Mungu ili kukabiliana na unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje. Matumizi ya maneno ya kumrejelea Mungu huwaliwaza *chokoraa* na kuwawezesha kujipa moyo kuwa yupo anayewapenda na kuwajali. Hii ina maana kuwa *chokoraa* huchukulia kuwa watu wengine hawawapendi ila Mungu anawapenda. *Chokoraa* hupitia changamoto nyingi zikiwamo ukosefu wa chakula na mahali pa malazi na unyanyapaa

kutoka kwa wanakundi-nje. Hali hii huwalazimu *chokoraa* kuwa na ukakamavu ili wasiathirike zaidi na chukulizi hasi kutoka kwa wanakundi-nje.

Hali na mazingira ndiyo hutofautiana baina ya *chokoraa* na wanakundi-nje. Ingawa hivyo, wapo watu ambao hawapendi kutangamana na *chokoraa* na ndiyo maana wao hutumia mikakati mbalimbali ya kilugha kukabiliana na unyanyapaa huo zikiwamo kuwadhalilisha kwa kuwatukana na pia kurejelea majina ya Mungu kuashiria kuwa anawajali. *Chokoraa* hujiliwaza kwa matumizi ya maneno yanayorejelea Mungu kwa kuamini jaala na kuwa anawajali pia kama afanyavyo kwa watu wengine. Imani hii huwapa ari ya kuvumilia changamoto wazipitiazo hasa unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje kama inavyobainika katika mazungumzo yafuatayo baina ya *chokoraa* wa jinsia ya kike wa Mathare, eneo la Mashimoni:

1. Mtu 1: **Mrembo sasa?**
2. Mpita njia: **Mmmmh**
3. Mtu 1: **Mbona sasa unaitikia kimadhash (***kimadharau***) hivyo? (**mpita njia hajibu na anaendelea na safari yake**) Kwani unadhani sisi sio watu? Unatuona kama machokosh (***chokoraa***) wachafu ambao hawana maana? Unaringia nini sasa na sote tulitoka kwa Jah (***Mungu***)?**
4. Mtu 2: **Aaai, iza (***poa***) mama, kwani umesahau kuwa sote tutadedi (***tutakufa***) tu. Hawa watu wanadhani kuwa Mungu anawalinda tu wao. Hata hajui anaeza enda hapo kwa daraja akutane na risasi akufe.**
5. Mtu 1: **Yenyewe mi hushangaa kwa nini hawa watu hujiona na sisi wote ni Sir God (***Mungu***) alituumba na hata sisi anatujali.**

Lugha katika mazungumzo haya inadhihirisha namna *chokoraa* wanavyokabiliana na unyanyapaa. Mpita njia wa jinsia ya kike hakuwapa *chokoraa* fursa ya kuzungumza naye bali aliwapita tu bila hata kujibu salamu zao kwa namna inayofaa. **Mtu 1** anamsalimia mpita njia kwa kutumia jina la kusifu. Ingawa hivyo, mpita njia anamjibu visivyo hali inayodhihirisha unyanyapaa. Hali hii iliwafanya *chokoraa* kuchukulia kuwa mpita njia huyo aliwadharau. Hata hivyo **Mtu 1** anajiliwaza kwa kutumia neno linalomrejelea Mungu anaposema kuwa "**…….sote tulitoka kwa Jah?**" Usemi huu unaonesha kuwa mtafitiwa huyu anajua kuwa Mungu ndiye

muumba wa watu wote na hivyo haina haja ya kubagua. Neno *Jah* linatumika kimkakati ili kujiliwaza dhidi ya unyanyapaa kutoka kwa mpita njia. **Mtu 1** anaelekea kukasirishwa na unyanyapaa kutoka kwa mpita njia ila **Mtu 2** anamliwaza kwa kumwambia kuwa "**Aaai, iza mama, kwani umesahau kuwa sote tutadedi tu. Hawa watu wanadhani kuwa Mungu anawalinda tu wao…...**"

Mazungumzo ya *chokoraa* yanadhihirisha kuwa wao hujiliwaza kwa kuamini kuwa watu wote ni sawa licha ya kuwa wao wanaishi mitaani huku watu wengine wakiishi nyumbani. Matumizi ya majina yanayorejelea Mungu yanabadilisha mtazamo hasi kwa kujua kuwa ingawa watu wengine wanawabagua kwa misingi ya hali za maisha, Mungu anawapenda na kuwajali. Hili linadhihirika pale **Mtu 1** anaposema kuwa "**………..na sisi wote ni Sir God alituumba na hata sisi anatujali.**" Katika usemi huu, matumizi ya maneno yanayorejelea Mungu yametumika kimkakati kwa kuwa yanawapa moyo *chokoraa* kwa kuamini kuwa Mungu ni mkuu kuliko changamoto zao.

Wazo kuwa Mungu anawapenda husaidia katika kupunguza msongo wa mawazo ambao hutokana na unyanyapaa. Kwa hali hii basi, tunaweza kusema kuwa imani kuwa Mungu anawajali huwapa matumaini maishani. Ni kwa misingi hii ambapo tunasema kuwa *chokoraa* wanaamini kuwa Mungu yupo na anawalinda kama afanyavyo kwa wanakundi-nje. Tumebaini kuwa *chokoraa* wa jinsia ya kiume hutumia maneno yanayorejelea Mungu kwa nadra sana. Tumebaini kuwa wao hutumia majina ya Mungu wanapozungumzia hatima yao kama inavyojitokeza katika mazungumzo yafuatayo, eneo la Mashimoni:

1. Mtu 1: **Sisi machokosh (***chokoraa***) jo tunaishingi tu kama wild animals (***wanyama wa mwituni***).**
2. Mtafiti: **Mbona unasema hivyo brathe (***ndugu***)?**
3. Mtu 1: **Aki vile sisi hulala tu nje na popote usingizi inatushikia tu tunalala.**
4. Mtu 2: **Yenyewe hapo umesema ukweli. Manze machokosh (***chokoraa***) tunakuwanga mahardcore (***wavumilivu***) sana. Msupa (***mrembo***) kama wewe hata haweziishi hii life (***maisha***) atoboe.**
5. Mtafiti: **Uko sure (***hakika***) sitatoboa?**

6. Mtu 1: **Manze huwezi na shukuru uko na home (***nyumbani***) kwenu.**
7. Mtu 2: **Hapa ni kukaa rada (***makini***), bure utajikuta hauna kakitu kakudish (***kula***) au ubambwe (***ushikwe***) na makarao (***polisi***).**
8. Mtu 1: **But (***ingawa***), hata sisi siku moja tutabahatika tu. Sir Jah (***Mungu***) atatusaidia.**
9. Mtu 2: **Yenyewe Sir Jah (***Mungu***) hata anawezafanya mmoja wetu akuwe tu MCA.**
10. Mtu 1: **Yenyewe kesho tunawesmake (***faulu***) na tuomoke (***tutajirike***) na Sir Jah (***Mungu***).**

Katika mazungumzo haya *chokoraa* wametumia lugha mkakati kwa kuamini kuwa Mungu ana uwezo wa kubadilisha hali yao ya maisha ya kesho. *Chokoraa* katika diskosi hii wanazungumzia changamoto wazipitiazo hasa za kuishi katika mazingira ambayo siyo ya kuridhisha. Lugha katika usemi wa **Mtu 1** inaashiria ulinganisho ambapo analinganisha maisha yao na wanyama. Hili linajitokeza anaposema kuwa "**Sisi machokosh jo tunaishingi tu kama wild animals.**" Usemi huu unaonesha kuwa *chokoraa* huishi kama wanyama wa mwituni ambao hula kile wanachoambulia. *Chokoraa* hurejelea majina ya Mungu wakati ambapo wanazungumzia maisha yao ya baadaye na kuonesha kuwa hali yao inaweza kubadilika. Hii ina maana kuwa hawajakata tamaa ya maisha mema licha ya kuwa wanaishi katika mazingira duni. Kulingana na mazungumzo haya ni wazi kuwa *chokoraa* wanaamini kuwa uwezo wa kuwa mtu wa kutajika katika jamii hutoka kwa Mungu. Matumizi ya majina yanayorejelea Mungu ni mkakati tosha wa kujiliwaza dhidi ya unyanyapaa unaotokana na watu wa makundi mengine ya kijamii. Ingawa hivyo, *chokoraa* wa Mathare pia hutumia mkakati wa kutumia lugha ya kuwadhalilisha wanakundi-nje ambao huwaambaa ili kujiliwaza kuwa kila mtu ana kasoro zake hasa za kimaumbile kama inavyobainika katika kisehemu kifuatacho.

**Matumizi ya lugha ya kudhalilisha kama mkakati wa kukabiliana na unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje**

Wakati wa kukusanya data kwa ajili ya utafiti huu tulibaini kuwa wapo wanakundi-nje ambao huwaambaa *chokoraa* kiasi cha kutotaka kuzungumza nao. Tumebaini kuwa *chokoraa* hutumia pia lugha ya kuwadhalilisha wanakundi-nje kama mkakati wa kupambana na unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje. *Chokoraa* hutumia lugha ya matusi kwa nia ya kudhalilisha wanakundi-nje wanaowaambaa. Huu ni mkakati muhimu kwa kuwa huwawezesha watafitiwa kuamini kuwa kila mtu ana kasoro kama wao. Kwa hivyo basi, matumizi ya lugha ya kudhalilisha wanakundi-nje hukusudiwa kuonesha kasoro zao na kuashiria kuwa wao pia siyo wakamilifu ingawaje wanaishi maisha bora nyumbani kwao ikilinganishwa na *chokoraa* ambao huishi mitaani.

Matusi, kwa mujibu wa makala hii ni maneno ya kuudhi wakati mtu hajaridhishwa na kitendo cha mtu mwingine. *Chokoraa* huishi katika mazingira duni ambayo hayazingatii kaida za kijamii na heshima. Mitaani wanamoishi hawapati kufunzwa kuhusu kaida hizi za kijamii bali hufunzwa mikakati ya kukabiliana na changamoto za maisha katika mazingira yao. Ni kwa sababu hii ambapo *chokoraa* hutumia lugha ya matusi bila kujali na wala hawachukulii kuwa ni kosa wala usimbeko. *Chokoraa* wa jinsia ya kiume hutumia maneno ya matusi zaidi ikilinganishwa na wenzao wa jinsia ya kike. Hali hii inabainika katika mazungumzo yafuatayo baina ya *chokoraa* wa Mathare, eneo la Mashimoni na mpita njia:

1. Mtu 1: **Sasa aunty. (**kimya**)**
2. Mtu 2: **Hawa mamasa (***akina mama***) wanapenda kujiringa sana.**
3. Mtu 3: **Yaani unaitwa unaringa, huwezi hata kuitikia tu salamu ya Mungu?**
4. Mtu 1: **Unaringa na hata huna sura, sisi huongea hata na maslay queen (***wasichana wa kisasa***) na haturingi.**
5. Mtu 3: **Na vile uko na haga zimesag (***makalio mazito***) vibaya vibaya.**
6. Mtu 2: **Afadhali usiringe coz hauna sura.**
7. Mtu 3: **Wachana na huyo mumama anajiduu (***anaringa***) tu bure.**
8. Mtu 2: **Unajua anatuona kama watu bure tu. Yeye ni fala (***mjinga***) sana.**
9. Mtu 3: **Ufala (***ujinga***) tu ndiyo ako nayo. Anafikiria tunamtaka sisi.**

*Chokoraa* wametumia lugha ya matusi kimkakati katika mazungumzo haya kwa kuonesha kasoro za mpita njia ambaye anakataa kujibu salamu zao. *Chokoraa* hapa wanachukulia kuwa mama mpita njia amekataa kujibu salamu zao kwa sababu ya hali yao ya kuishi mitaani na hivyo basi wakaamua kujiliwaza kwa kumdhalilisha kwa kurejelea maumbile yake. Matusi katika mazungumzo haya yametumika kimkakati kwa nia ya kuonesha kasoro za kimaumbile za mpita njia. *Chokoraa* wanatumia matusi kumdhalilisha na matusi haya yanakuwa kama liwazo dhidi ya unyanyapaa unaotokana na wanakundi-nje kuwabagua na kukataa kujibu hata salamu zao.

Usemi huu wa **Mtu 3** kuwa «**Anafikiria tunamtaka sisi**» unaashiria kuwa *chokoraa* hawakuwa na la ziada kwa mpita njia ingawa alikataa kuwasikiliza. Maneno haya ya kumdhalilisha mpita njia yanakuwa liwazo kwa *chokoraa* kwa kuonesha kuwa ingawa hakujibu salamu zao, wao hawakuwa na haja naye na pia yeye ana kasoro za kimaumbile. Diskosi hii ya *chokoraa* wa jinsia ya kiume ina maneno ya matusi katika kila usemi isipokuwa usemi wa kwanza ambao ni salamu. **Mtu 2** anatumia lugha ya matusi katika kipengele cha pili anaposema kuwa «**wanapenda kujiringa sana.**» Neno *kujiringa* ni matusi na mtafitiwa analitumia baada ya mwanakundi-nje kukataa kujibu salamu zao. Nia yao ya kujiliwaza inatimizwa licha ya kuwa wanakiuka kaida za jamii. *Chokoraa* hapa wametumia matusi yanayogusia maumbile ya warejelewa wao wa kike zikiwamo sehemu za siri kama vile makalio, kama inavyodhihirika **Mtu 3** anaposema kuwa **«Na vile uko na haga zimesag vibaya vibaya.»** Nia kuu ya *chokoraa* huyu ni kuonesha namna mama huyu alivyo na kasoro za kimaumbile na kwa sababu hiyo hapaswi kuwachukulia *chokoraa* kama watu duni.

Tumebaini kuwa *chokoraa* wa jinsia ya kike hutumia matusi yasiyohusiana na maumbile ya mtu. Wao hurejelea hali ya mtu zaidi ikilinganishwa na maumbile yake. Kwa maoni yetu, *chokoraa* wa jinsia ya kike hujaribu kutumia lugha isiyo chafu sana ikilinganishwa na wenzao wa jinsia ya kiume. Kwa sababu hii basi, tunaweza kusema kuwa *chokoraa* wa jinsia ya kike hutumia maneno ya tasfida hata wanapotumia lugha ya kudhalilisha kujiliwaza dhidi ya unyanyapaa. Hali hii inabainika katika mazungumzo yafuatayo miongoni mwa *chokoraa* wa jinsia ya kike katika eneo la Gitathuru:

1. Mtu 1: **Hawa wamama wa soko wanakuwanga na ufala mingi sana.**
2. Mtu 2: **Walikufanyia?**
3. Mtu 1: **Imagine (***fikiria***) wanadai ati sisi ndiyo tunawafukuzia kastoma.**
4. Mtu 2: **Aje sasa tena?**
5. Mtu 1: **Ati vile tunakaa mahali kastoma wanapita na wanatuogopa.**
6. Mtu 3: **Kwani tunaogopwa tuko na ukoma au tumededisha (***tumeua***) mtu. Huo ni ushetani wao tu.**
7. Mtu 2: **Ujinga ndiyo mingi kwa hii mtaa.**

*Chokoraa* wanatumia lugha ya matusi katika mazungumzo haya kwa sababu ya unyanyapaa kutoka kwa wanakundi-nje. Maneno ya matusi ambayo yametumika hapa ni '*fala*', '*ujinga*' na '*ushetani*'. Maneno haya ni ya kidhahania tu na wala hayatokani na namna mtu anavyoonekana. Lugha hii ya matusi katika diskozi ya *chokoraa* wa jinsia ya kike ni tofauti na ile ya wenzao wa jinsia ya kiume.

*Chokoraa* pia hutukanana wenyewe kwa wenyewe. Matusi baina ya watu wa jinsia ya kike kwa jinsia ya kiume yanahusu ukosefu wa uwajibikaji kama vile kuwa mwanamme bwege asiye na faida katika jamii. Kwa upande mwingine, *chokoraa* wa jinsia ya kiume hutumia matusi yanayorejelea kasoro za kimaumbile kwa wenzao wa jinsia ya kike kwa nia ya kuathiri hisia zao kwa njia hasi hasa baada ya kukataliwa kimapenzi kama inavyobainika katika diskozi ifuatayo ya eneo la Mashimoni:

1. Mtu 1: **Wewe kuro** (*kahaba*) **tutapelekana wapi?**
2. Mtu 2: **Fala hii, jione kwanza, ati kuro** (*kahaba*) **nililala…..**
3. Mtu 1: **Unajifanya baabi** (*mtu wa maana*) **na huoni umekuwa mshosho** (*ajuza*).
4. Mtu 2: **Wewe funde** (*mjinga*) **achana na mimi, siku…..**
5. Mtu 1: **Mkundu hii unafikiria nakumezea** (*nakutamani*)?
6. Mtu 2: **Ulikuwa unataka nini kama si kunimezea**?
7. Mtu 1: **Sitaki upoko** (*ukahaba*) **wako hapa**, (akimsogelea) **nitokee au nikupee beat** (*kichapo*).
8. Mtu 3: **Cheza chini, cheza chini** (*acha, acha*)

9. Mtu 2: **Kimtu kazi yake ni mnonyi** (*pombe*) **akili yake……**

Diskozi hii ni kielelezo cha matumizi ya lugha ya kudhalilisha kwa sababu ya kukataliwa kimapenzi. **Mtu 1** na **Mtu 3** ni *chokoraa* wa jinsia ya kiume huku **Mtu 2** akiwa mwenzao wa jinsia ya kike. **Mtu 1** anamtusi **Mtu 2** kuwa yeye ni kahaba na haiwezekani wawe na uhusiano wa kimapenzi baina yao. Kutokana na maneno ya **Mtu 2** ni wazi kuwa **Mtu 1** alikuwa amemtongoza ila kwa kuwa alimkataa, anamtusi kwa kutumia maneno ya Sheng' kama vile '*kuro*' na '*poko*' yaliyo na maana ya kahaba. Matumizi ya lugha ya **Mtu 1** yanaashiria kuwa uhusiano baina yake na **Mtu 2** hauwezi kuendelea kama mkakati wa kujiliwaza dhidi ya kukataliwa kimapenzi. Mtafitiwa ana nia ya kuashiria kuwa hana haja na mwenzake wa jinsia ya kike anapomwita kahaba. Kwa upande mwingine, **Mtu 2** anasema kuwa **Mtu 1** ni mjinga na anayependa kubugia pombe. **Mtu 2** anatumia matusi ya kurejelea hali kama vile ujinga na ulevi ilhali **Mtu 1** anatumia matusi ya kurejelea maumbile anapotumia neno *mkundu*. Matumizi ya maneno ya matusi hapa ni mkakati wa kilugha unaotumiwa na *chokoraa* kwa nia ya kudhihirisha sababu za kukataliwa kimapenzi. Sababu wanazozitoa zinaashiria namna kila mmoja wao anavyotaka kutimiza nia ya kuonesha ubaya wa mwenzake na hivyo basi kuthibitisha sababu zake za kukataa mahusiano baina yao.

**Hitimisho**

Katika makala hii tumeonesha kuwa *chokoraa* wa Mathare hutumia lugha mkakati kwa sababu kama vile: kwanza, kuchanganya ndimi ili kutumia maneno ya lugha fulani ambayo yana athari kuu kwa wazungumziwa na hatimaye kutimiza nia ya kupata msaada. Pili, matumizi ya uradidi kwa nia ya kusisitiza yanayosemwa. Tatu, *chokoraa* wa Mathare hutumia lugha ya kuwadhalilisha wanakundi-nje na pia kurejelea majina ya Mungu kama njia mojawapo ya kujiliwaza dhidi ya unyanyapaa. Tumeangalia mawasiliano ya *chokoraa* wa Mathare ya kutimiza nia zao za wakati husika kwa kurejelea mifano inayodhihirisha matumizi ya lugha mkakati.

**Marejeleo**

Christopoulos, D. (2010). *Peer Esteem Snowballing: A Methodology for Expert Surveys*. IUSS Press.

Maritza, R. M (2016). Communication Strategies Used by Different Level L2 English Learners in Oral Interaction. *Revista Signos.Estudios De Linguistica ISSN0718-0934, 2016 Pucv, Chile.*

Maleki, A. (2007). Teachability of Communication Strategies. *An Iranian Experience System*, 35(4), 583-594.

Muriira, M. P. (2016). A Complex Linguistic Code in Kenyan Linguistic Scene: A Case Study for Sheng. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Njiru, R. (2005). Survival Strategies and their Implications for The Reproductive Health of Street Girls in Nairobi. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Selinker, L. (1972). Interlanguage. *IRAL, 10(3), 209-231*

Suda, C. (1997). Street Children in Nairobi and the African Cultural Ideology of Kin-based Support System: Change and Challenge. *Child Abuse Review Vol. 6*

Tarone, E. (1977). Conscious Communication Strategies In Interlanguage: A Progress Report. *In H. Douglas Brown, C.A. Yorio And R.H. Crymes (Eds), TESOL'77: Teaching And Learning English As A Second Language pp.194-203. TESOL.*

Varadi, T. (1973). Strategies of Target Language Communication: Message Adjustment. *Paper Presented At The V1 Conference of The Rumanian-English Linguistics Project, Timisoara.*

Warambo, J. P. (2011). Uchanganuzi wa Maendeleo ya Kisemantiki katika Sheng': Mtazamo wa Pragmatikileksika. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).

Yang, D. na Gai, F. (2010). Chinese Learners Communication Strategies Research: A Case Study at Shandong Jiaotong University. *Cross-Cultural Communication, 6(1), 56-81*.